
CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO - TPS SACCOS LTD



PICHA

FOMU YA MKATABA MKOPO WA MAENDELEO.

N.B. FOMU HII IJAZWE NA KUKAMILISHWA KWA HERUFI KUBWA TU

Makubaliano haya yapo kwa mujibu wa Kanuni ya Sheria Ndogo ya Fedha ya mwaka 2019 S. 39 (1) – (2) na sera ya mikopo ya chama.

MAKUBALIANO HAYA YANAINGIWA KATI YA TPS SACCOS LTD NA.

Majina Matatu			
Ninakopa Tshs	Kwa Muda wa Miezi		
Kwa Rejesho la Mwezi Tshs	Jumla ya Mkopo Wote ni Tshs		

Kwamba ninakopa Mkopo wa Maendeleo kwa masharti yafuatayo:-

1. Ninaomba mkopo kwa riba ya 10% kwa Njia ya Ulalo “Reducing Balance Method”
2. Kulipa 1.5% ada ya mkopo na 1% Mfuko wa Majanga ya mkopo nilioomba na fedha hizo zitakatwa mara moja kwa mkupuo mwanzoni mwa mkopo kabla sijalipwa.
3. 1% ya Mfuko wa Majanga ninayokatwa ***itanikinga tu*** endapo nitapatwa na janga la kifo au ulemavu wa kudumu utakaopeleka kushindwa kulipa deni langu. Majanga mengine yote ambayo hayajatajwa katika fomu hayausiki na Mfuko wa Majanga huu.
4. Ninatambua kiwango cha chini cha mkopo ni kuanzia **Tshs 1,000,000 – 70,000,000**.
5. Natambua malipo ya mkopo huu ni kupitia mshahara wangu hadi deni langu litakapomalizika. Dhamana ya mkopo ninaoomba ni utumishi wangu ndani ya ***Jeshi la Magereza au taasisi niliyopo***. Endapo ni mwenza wa mtumishi, dhamana ya mkopo ninaoomba itakuwa ni ***utumishi wa mwenza wangu*** hadi deni langu litakapomalizika na mwenza wangu atatakiwa kuwa ***Mdhamini Na. 1.***

6. Endapo utumishi wangu utakoma ndani ya Jeshi la Magereza kwa sababu zozote zile kama **KUSTAAFU, KUFUKUZWA KAZI, KUACHA KAZI, KUSIMAMISHIWA MKATABA** na nyinginezo na kupeleka kushindwa kumalizia kulipa deni lillobaki pamoja na riba yake baada ya kutumia akiba zangu kulipa deni hilo, kwa mkataba huu ninatoa kibali kwa **MAMLAKA HUSIKA** kukata salio la deni langu lote kutoka kwenye stahiki zangu zote hadi litakapomalizika. Mamlaka hizo zinaweza kuwa **Jeshi la Magereza, PSSSF, NSSF** au asasi zote za kifedha ambazo nitakuwa na akaunti au maslahi yangu yanapitia.
7. Nitaruhusiwa kuomba TOP – UP endapo nitakuwa nimehudumia nusu ($\frac{1}{2}$) ya muda niliyoomba mkopo na nitapewa punguzo au msamaha wa riba yote iliyobaki.
8. Endapo nitaamua kulipa deni langu la mkopo kwa kununuliwa na taasisi nyingine za kifedha au kulipa deni langu nje ya mfumo wa TOP – UP, sitapewa punguzo au msamaha wowote wa riba iliyobaki.
9. Endapo kwa sababu zozote zile makato ya mkopo yatakuwa hayajaanza kuanzia miezi mitatu na kuendelea tokea kukamilika malipo ya mkopo huu, nitawajibika kutoa taarifa chamani ili makato hayo yaanze mara moja.
10. Endapo kwa sababu zozote zile kutakuwa na makosa katika uingizaji wa deni langu katika mfumo kama kutobadilishwa kwa deni endapo ni TOP – UP, kuingiziwa rejesho dogo au lisilo sahihi na mengineyo nitazalimika kutoa taarifa chamani kwa ajili ya usuluhishi.
11. Itahesabika nimefanya kosa la kinidhamu endapo nitagundua kasoro zilizoelezwa katika kifungu 09 – 10 na kuamua kuzichukulia faida kasoro hizo kwa kukopa kwenye taasisi nyingine za fedha. Endapo nitafanya hivyo, na chama kugundua kasoro ya mkopo wangu, ninakiruhusu chama kuchukua hatua sahihi ambazo zitawezesha mimi kulipa deni langu lote ikiwa ni pamoja na kuingiza upya makato yangu kwenye mfumo. Ikiwa makato yatagoma, ninatoa kibali kiasi cha rejesho kilichogoma kikatwe moja kwa moja kupitia Posho ya Chakula, “Package” hadi deni langu litakapomalizika.
12. Ninatambua kwa mujibu wa sera za chama salio la mkopo uliocheleweshwa kwa kupita muda wake utatozwa adhabu ya 5% ya salio la marejesho yaliyocheleweshwa.
13. Nitawasilisha fomu moja ya maombi ya mkopo wa maendeleo ikiwa pamoja na mkataba wake chamani. Fomu hii itafika chamani ikiwa aidha ni nakala halisi “Original” au nakala ya fomu iliyoscaniwa vizuri na “scanner” na

siyo simu kwa njia ya E- Mail ya chama. Nakala moja pamoja na mkataba itabaki kituo cha mwanachama kwa kumbukumbu.

14. Kasoro yoyote itayojitokeza nje ya kifungu 1 – 14 ya mkataba huu itasuluhishwa kwa njia ya majadiliano kati ya **MKOPAJI** na **MKOPESHAJI** ambaye ni **TPS – SACCOS LTD.**

TAMKO LA MKOPAJI

Nakiri kwamba nimesoma na kuyaelewa masharti yote yaliyomo katika mkataba huu na maelezo yote niliojaza katika fomu ya maombi ya mkopo wa maendeleo na mkataba huu ni kweli tupu na endapo nitakiuka makubaliano ya mkataba huu hatua za kisheria stahiki zichukuliwe dhidi yangu.

MAJINA MATATU YA MWANACHAMA	SAHIHI	TAREHE

KWA MATUMIZI YA OFISI TU

MAJINA KAMILI YA SHAHIDI WA MKOPESHAJI			
SHAHIDI WA MKOPESHAJI		SAHIHI.	
TAREHE			

FOMU AMBAYO HAITAJAZWA KIKAMILIFU HAITASHUGHULIKIWA
